# Hali ya Uoga

TotalEnergies inahusishwa na ukandamizaji wa walinzi wa ardhi na mazingira Afrika Masharik

**desemba 2023**



Jjumba Martin / Global Witness

## Table of contents


**Utangulizi** ........ 3

**Vitisho vilivyoripotiwa, ucheleweshaji na fidia ndogo** ........ 5

**Mafuta ya Uganda: Mradi wa kibinafsi wa Dikteta** ........ 8

Wafanyakazi wa kampuni na wanakandarasi wanadaiwa kuhusishwa na vitisho ........ 9

Harakati chini ya ulinzi nchini Uganda ........ 12

Matendo ya Kulipiza Kisasi dhidi ya wakosoaji wa TotalEnergies ........ 15

Kesi kadhaa za watu kukamatwa ........ 16

**Tanzanie : suppression de l'espace civique** ........ 17

**Kudhoofisha Uwajibikaji** ........ 19

**Athari ya Kutamausha** ........ 20

**Hitimisho** ........ 21

**Mapendekezo** ........ 22

Nchi za Uganda na Tanzania ........ 22

Kampuni ya TotalEnergies ........ 23

Taasisi za Fedha Duniani ........ 24


Umoja wa Ulaya ........ 24

## Utangulizi

Mara ya kwanza Kampuni ya mafuta ya Total Energies ilitembelea kijiji cha Swalehe Nkungu, mwaka wa 2018 nchini Tanzania, Swalehe na majirani wake waliahidiwa kulipwa fidia nzuri kwa sababu ya mashamba yao. Miaka mitano baadaye, Swalehe alisema alilindwa kwa silaha kali na kulazimishwa kutia saini mkataba ambao hakuruhusiwa kusoma na uliokuwa na fidia ndogo kinyume na makubaliano ya awali. Swalehe alisema fidia hiyo haikutosha kununua shamba lingine. Alitumia pesa hiyo kuikimu familia yake ya watoto kumi na wawili na kununua chakula. "Sasa hatuna chochote," Swalehe alisema.

Juhudi zake za kutafuta usaidizi kutoka kwa mashirika ya kiraia ya Tanzania, zimekabiliwa na vitisho na unyanyasaji kutoka kwa walio mamlakani. Mara tatu katika mwaka uliopita, mkulima huyo mwenye umri wa miaka 48 alihojiwa na maafisa wa serikali kuhusu uhusiano wake na mashirika ya kiraia.

Asubuhi ya kufika nyumbani kutoka mkutanoni wa mashirika ya kiraia mnamo Februari 2023, aliitwa kwenye ofisi ya afisa wa serikali. Akiwa peke yake ndani ya chumba, kwa muda wa masaa matatu, Swalehe alihojiwa na afisa wa serikali pamoja na afisa wa upelelezi kuhusu safari zake na juhudi zake za kupinga mradi wa mafuta uliopangwa kufanywa. Walimuonya akome tabia hizo na kumtishia kumnyang'anya pasipoti yake. Swalehe aliambia Global Witness.





**Bomba hilo lenye urefu wa kilomita 1,443 litapita katika makazi ya wanyamapori, maeneo ya hifadhi na mashamba ya asili.**

Swalehe ni mmoja miongoni mwa makumi ya watu wanaokabiliwa na changamoto kama hiyo kwa kuchukua msimamo dhidi ya kampuni ya mafuta ya Ufaransa ya TotalEnergies inayopanga kujenga bomba la mafuta ghafi yenye joto katika Afrika Mashariki wakiazimia liwe ndilo bomba refu zaidi duniani.

Bomba hilo la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lenye thamani ya dola za Marekani bilioni 5, litachukua sehemu ya ardhi ya kilomita 1,443 kutoka magharibi mwa Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania, ambapo litasafirishwa kwa wanunuzi wa kimataifa.  Kiwanda cha mafuta cha Tilenga, ambacho huchimba mafuta katika hifadhi ya taifa, kitasambaza mafuta kwenye bomba hilo. Kwa pamoja, miradi hiyo inapitia kwenye makazi ya wanyamapori, maeneo ya hifadhi na mashamba ya asili na  itaathiri zaidi ya watu 100,000.  Mradi huounakadiriwa kutoa tani milioni 379 za gesi aina ya CO2 katika muda wa miaka 25 utakaokuwa hapo –  hii ni nyingi sana ikilinganishwa na iliyotolewa Uingereza gesi iliyotolewa mnamo 2022. Ujenzi wa bomba hilo ulianza mwaka wa 2023 baada ya kucheleweshwa sana.

Bomba hilo na kiwanda cha mafuta cha Tilenga zinafadhiliwa na kampuni ya TotalEnergies, ambayo imeshirikiana na kampuni mbili za mafuta zinazomilikiwa na serikali - Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) vilevile Shirika la Mafuta la China la Overseas (CNOOC).




**Bomba hilo na kiwanda cha mafuta cha Tilenga zinafadhiliwa na kampuni ya TotalEnergies**

Global Witness waliungana na Taasisi ya Utafiti ya Tasha (Tasha Research Institute) nchini Uganda na Green Conservers nchini Tanzania kuchunguza ushiriki wa makampuni yanayotaka kukomesha watetezi wanaopinga ujenzi wa bomba hilo.

Uchunguzi wetu unatokana na mahojiano na zaidi ya watu 200 walioathiriwa na mradi huo wa bomba, wanaharakati, waandishi wa habari na wataalamu pamoja na uchambuzi wa vyombo vya habari na ripoti za umma pamoja na ripoti za mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya kiraia na mahakama.

Matokeo yetu yanaonyesha kuwa hali ya hofu nchini Uganda na Tanzania inazuia mashirika ya kiraia na wanajamii kupinga mradi huo. Wawakilishi wa TotalEnergies, wanakandarasi na washirika wa biashara wameripotiwa kushinikiza watu kukubali viwango vya fidia visivyofaa kwa mashamba yao. Pia, mawakala wa serikali wanaendeleza kampeni ya vitisho na kuwakomesha wanaharakati wa hali ya hewa na mashirika ya kiraia ambayo yanatetea familia zilizohamishwa.

Hatua kali zaidi za kimataifa zinahitajika ili kulinda watetezi wa mazingira na haki za binadamu kama sehemu ya mazungumzo ya hali ya hewa yanayoendelea katika COP 28 huko Dubai.

Wakijibu kupitia kwa mawakili, TotalEnergies walikanusha vikali pendekezo lolote kwamba: wamekiuka majukumu yao kuhusu biashara na haki za binadamu, wamewanyanyasa wanajamii ili kukubali makazi yasiyofaa, wamefanya lolote ili kuleta hali ya hofu katika jamii zilizoathiriwa ama wakayapa masilahi yao ya kifedha kipaumbele kuliko jamii na mazingira.

## Vitisho vilivyoripotiwa, ucheleweshaji na fidia ndogo

Wanajamii wengi tuliowahoji nchini Tanzania na Uganda wanasema walidanganywa kwa kupewa hela kidogo katika mchakato wa kutwaa ardhi. Mchakato wa fidia ulicheleweshwa sana, kwa sehemu kutokana na janga la COVID-19, pia, tarehe za makataa ziliwekwa ambazo zilizuia watu kutumia mashamba yao kwa uhuru ama kukuza mazao ya kudumu yenye faida zaidi.[1] TotalEnergies iliripoti kuwa katika visa vingi fidia haijalipwa kwa sababu ya ucheleweshaji.

Watu walisubiri kwa miaka mingi kulipwa fidia zao na kufikia wakati huo walisema bei ya mashamba karibu na njia ya sehemu ya mradi wa bomba ilikuwa imepanda - ikichochewa na kukisia kwa bei ya ardhi, waliponunua kwa bei ya chini – wanajamii walishindwa kufikia bei hiyo. Wengi walisema kuwa kwa sababu hiyo hawakuweza kumudu kununua mashamba mengine kwa fidia iliyotolewa. Pia, wanajamii walisema hawakuhusishwa katika mchakato wa kufanya maamuzi na uthamini wa mashamba hayo jambo lililosababisha mazao na mali yao kutothaminiwa.[2]

Nchini Tanzania, ambapo sheria inaeleza kuwa rais anamiliki mashamba yote na watu wana haki ya matumizi ya kimila tu, inaweza kuwa vigumu zaidi kukataa utwaaji wa mashamba. Watu wengi walisema wamezidi kuwa masikini na sasa wanatatizika kuishi kwa sababu ya mradi huo.

Mradi uliendelea licha ya madai ya umma ya mchakato wa utwaaji wa mashamba kwa lazima, ukiambatana na ucheleweshaji, mawasiliano duni na fidia ndogo kwa familia.

TotalEnergies, wanakandarasi wao na washirika wao wa kibiashara, wameshutumiwa na vikundi vya kampeni vya taifa na kimataifa kwa kushinikiza, kunyanyasa na kutisha wanajamii ili wakubali mikataba mibaya.[3]

Tunaeleza kwa undani katika ripoti hii, Global Witness imegundua kuwa kuna ushahidi wa kuunga mkono shutuma hizi.

Walioshuhudia wanasema wafanyakazi wa kampuni wakati mwingine walisafiri kwa misafara mikubwa, wakati mwingine pia wakisindikizwa na polisi, jeshi na vikosi vya usalama vya kibinafsi, jambo ambalo lilitisha wanajamii zaidi.



**Leoniah Itho Okella alisema alishinikizwa kukubali fidia ambayo ilikuwa ndogo sana.**
Jjumba Martin/ Global Witness

"Tuliishi kwa hofu na kuishia kukubali pesa kidogo walizochagua kutupatia," mwanajamii mmoja kutoka Kikuube, Uganda, alieleza kwa ufupi jinsi walivyohisi kuhusu hali hiyo.

Hata hivyo, TotalEnergies, imekanusha kutekeleza "sehemu yoyote ya mchakato wa utwaaji wa ardhi mbele ya polisi, jeshi, au vikosi vya usalama vya kibinafsi."

Pia, kulikuwa na mambo yaliyodaiwa kwenye mkataba; kukosa kuzipa jamii muda wa kutosha kuelewa stakabadhi hizo au kutohakikisha zinatolewa kwa lugha zinazofaa. Nchini Uganda, mikataba ilikuwa ya Kiingereza tu, huku Tanzania, baadhi ya wanajamii wanasema walilazimishwa kutia saini mikataba papo hapo, bila hata kuisoma.

*"Watu walitia saini kwa kulazimishwa, walihisi hawana chaguo," Benon Tusingwire alisema; mkuu wa The Hoima- based group Navigators of Development Association (NAVODA).*

Takriban mtu mmoja kati ya watu watano nchini Uganda na Tanzania hawajui kusoma na kuandika, wengi wao wakiwa katika maeneo ya vijijini.[4] Hata hivyo, waliohojiwa na Global Witness walisema wanasheria na watafasiri walioteuliwa na kampuni pekee ndio waliokuwepo. Pia walisema kuwa, Wanasheria na watafsiri hao walikuwa wakiegemea upande wa serikali na kuongeza shinikizo zaidi kwa jamii. Mkulima mmoja Mtanzania alikumbuka akimhoji mwanasheria mmoja kuhusu viwango vya chini vya fidia, kisha akaambiwa: “Ikiwa una malalamishi yoyote, unaweza kupeleka serikali mahakamani.”



**Jamii za Buliisa, Uganda, zimeona mitambo ya kuchimba mafuta ikitokea karibu na mashamba yao.** *(Jjumba Martin / Global Witness)*

Wanajamii wanasema waliambiwa na maafisa wa kampuni na maafisa wa serikali - wakati mwingine wakiandamana na vikosi vya usalama - kwamba hawakuwa na chaguo ila kukubali viwango vya fidia vya chini, kwamba mradi huo ungeendelea kwa hali zote na kwamba hawana uwezo wa kulinda haki zao na kuongea lolote dhidi ya serikali. Wale waliokataa wanasema walitishiwa kuchukuliwa hatua za mahakama, na wakazidi kulazimishwa na makampuni na maafisa wa serikali. Waliambiwa msaada wao pekee ni kuchukua hatua za kisheria, ambazo mwishowe waliambiwa zitafeli na itawagharimu pesa nyingi.

> ***"Mara nyingi wanaambiwa, hakuna chochote mnaweza kufanya, hata mkipinga mtafukuzwa tu."***
> – Dickens Kamugisha, Dickens Kamugisha, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Afrika ya Utawala wa Nishati (AFIEGO)

Timu ya EACOP mjini Kampala ilikataa kwa Global Witness kwamba vitisho au unyanyasaji wowote ulifanyika na kusisitiza kuwa wanajamii walipewa fidia ya haki. Katika barua kwa Global Witness, TotalEnergies walisisitiza kwamba EACOP Ltd na kampuni zake tanzu, TotalEnergies E&P Uganda (TEPU) zilifuata viwango vilivyowekwa na Shirika la Fedha la Kimataifa na kwamba fidia ilitolewa kwa "gharama kamili na inayofaa" ama watu walipewa nyumba mpya za makazi. Katika mpango wao wa fidia ambao Total walisema walitumia:

*"ushahidi wa soko kama vile makubaliano ya hivi majuzi ya mauzo ya ardhi na uhamishaji ardhi [ambao] hukusanywa kutoka eneo la mradi ili kutoa data ya thamani. Vilevile, TEPU na EACOP Ltd zilikusanya taarifa kutoka kwa wawakilishi wa serikali za mitaa, wajumbe wa Kamati ya Ardhi ya Eneo, na wakazi wengine wa eneo hilo ambao walikuwa na ujuzi wa ardhi ya eneo hili na thamani za mali. Taarifa hii ilichambuliwa ili kufikia kiwango kinachofaa kwa kila eneo lililotengwa. Zoezi hili la utafiti lililenga wamiliki tofauti wa ardhi na aina tofauti za umiliki wa ardhi ndani ya vijiji maalum katika eneo la mradi. Wanajamii na washikadau walishirikishwa kikamilifu wakati wa mchakato wa uthamini, ambao umeandikwa vyema, na wahusika walioathirika walishughulikiwa kibinafsi kabla ya thamani kuamuliwa. Katika hali hizi ... malipo ya fidia hayangeweza kuwa - na, kwa kweli, hayakuwa - yanatoshana.*



**Kazi ya ujenzi wa bomba inayofanyika Hoima, Uganda.**
*(Jjumba Martin/ Global Witness)*

“Wanajamii walipewa "watu wa tatu" mawakili na huduma za tafsiri kwa mujibu wa sheria,” TotalEnergies walisema. "PAPs [watu walioathiriwa na mradi] ambao wanakabiliwa na changamoto katika kutafuta mashamba inayolingana na yao ya awali wameamua kuchagua mashamba ambayo yako mbali na eneo la mradi ambalo bei ya ardhi hapo iko juu," hayo yalikuwa maandishi kwenye barua hiyo. Pindi tu wauzaji wanapokubaliana kwa hiari na yaliyomo katika mkataba wa fidia, mipango inafanywa kutia saini na kurasimisha, haya yakisababisha kutia saini mbele ya mwenyekiti, mpenzi wa mtu anayetia saini (panapowezekana), Kamati ya Mipango ya Makazi mapya (RPC) au mwakilishi wa EACOP, shahidi mteule wa anayetia saini, mtafsiri na wakili. Pia, walidai kuwa, kujisajilisha kwa mipango ya fidia huendeshwa kwa takriban asilimia 95%, bila 'shurutisho' kutia saini chochote.

Mawakili wa TotalEnergies waliongeza kuwa kampuni yao ya mafuta haikuwajibika kwa hatua zozote zilizofanywa na serikali ama maafisa wa serikali na kwamba ununuzi wa shamba la kufanyia mradi wa bomba na mfumo wa kutoa fidia ulihusisha michakato ya uchunguzi. TotalEnergies imefanya "ahadi za wazi na za muda mrefu za kuheshimu haki za binadamu na mazingira," waliongeza. Pia, Global Witness walidokezewa kwamba mikakati ya kurejesha maisha ya awali inaendelea katika jamii zilizoathiriwa "kwa miaka mitatu... au hadi ambapo maisha hayo yatarejeshwa kikamilifu" na lengo "elimu ya kifedha, programu ya kilimo kwa ajili ya uboreshaji wa mazao na mifugo, vitalu, ufugaji nyuki, usimamizi wa fedha, ujuzi wa biashara na mafunzo ya ufundi ili kuwasaidia wanaotafuta kazi."

## Mafuta ya Uganda: Mradi wa kibinafsi wa Dikteta

Tangu mafuta yalipogunduliwa huko Albertine Rift nchini Uganda mwaka wa 2006, utumizi mbaya wa mafuta hayo umeashiria maazimio ya Rais Yoweri Museveni. Museveni, ambaye amekuwa mamlakani kwa zaidi ya miaka 37, ameielezea kama "mafuta yake"na akajenga mkakati wa maendeleo ya nchi

kupitia  wa mradi huo  Ametumia mamia ya mamilioni ya dola katika kuendeleza miundomsingi ya bomba hilo, ikiwa ni pamoja na kujenga barabara nyingi hali ambayo imeifanya nchi kuwa madeni mengi.[5]

Serikali ya Uganda imekosolewa kwa kukosa kuchapisha mkataba wake na TotalEnergies, huku kukiwa na madai ya ufisadi.  Kulingana na ripoti rasmi , iliyochapishwa mnamo 2022, karibu robo ya bajeti ya kitaifa inapotea kila mwaka kwa ufisadi.

Familia ya Museveni inaripotiwa kuhusishwa na kampuni zinazohusika na mradi huo wa mafuta, ikiwa ni pamoja na kampuni ya kibinafsi ya usalama ambayo inahifadhiwa na TotalEnergies, Saracen,[6] na hivyo kumpatia Rais mapato zaidi kwa nia ya kukandamiza upinzani dhidi ya mradi huo. Akizungumza katika uamuzi wa mwisho wa uwekezaji mwaka jana na Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa TotalEnergies Patrick Pouyanné kwenye hadhira, Museveni aliyataja mashirika yasiyo ya Serikali (NGOs) kama "watu wasio na maana" ambao wanapaswa kuachwa "walale msituni".

Waendeshaji wa serikali, ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Petroli ya Uganda (PAU), mamlaka za serikali za mitaa, vikosi vya usalama, ikiwa ni pamoja na polisi wa mafuta na gesi, wanahusishwa na dhuluma zinazoripotiwa dhidi ya jamii.

## Wafanyakazi wa kampuni na wanakandarasi wanadaiwa kuhusishwa na vitisho

TotalEnergies na kampuni zilizopewa kandarasi ya kusimamia mchakato wa utwaaji wa ardhi nchini Uganda, Atacama na NewPlan zimeshutumiwa kwa shinikizo na vitisho. Mashahidi wanasema wamejihusisha na mikutano ya mashirika ya kiraia, wakazunguka ili kutafuta taarifa kuhusu wafanyakazi wa kujitolea wa jamii, na kuwaonya watetezi wa ardhi na mazingira dhidi ya kuwapotosha watu au kueneza habari "za uwongo".

Mashahidi watatu walielezea tukio la Aprili 2021 wakati afisa aliyejihami aliingia ghafla kwenye mkutano wa wanajamii katika Wilaya ya Rakai pamoja na mfanyakazi wa TotalEnergies.  Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa amealikwa. Mtu huyo aliyekuwa na silaha, aliyedai kutoka katika Wizara ya Nishati, aliwakashifu na kuwashutumu wanaofanya mkutano huo kwa kupotosha jamii. "Unawaambia wapinge mradi ", Florence Nakandi kutoka  Community Transformation Foundation Network (COTFONE) alikumbuka akiambiwa. "Usipoacha unachofanya tutaona nani ni nani."  Wanajamii walisimamisha mkutano wakihofia usalama wao.

Watetezi wanaoshikilia mkataba bora zaidi wanashuhudia ongezeko la vitisho.

Katika kisa kimoja, mwanakandarasi wa TotalEnergies anaonekana akimtisha mkulima aliyefungiwa kwenye mzozo na kampuni hiyo kwa kujenga ua uliouzunguka nyumba yake. Fred Balikenda alikataa kuhama, licha ya kile alichosema kuwa ongezeko la vitisho na shinikizo.  Kufuatia haya, mwanakandarasi huyo wa TotalEnergies alianza kujenga ua ambao ulimtenga Fred na majirani wake na pia kumtenga na choo chake.  Fred alisema inahisi kama anaishi "gerezani" na pia akasema kwamba amekuwa akitishwa na maafisa wa serikali

wanaofanya kazi na Total kwenye mradi huo.  TotalEnergies walikanusha kumtisha Balikenda na kusisitiza kuwa ua huo ulijengwa kwa idhini yake na kwa "usalama" wake.



**Fred Balikenda amezungushiwa ua na mwanakandarasi wa TotalEnergies.** *Jjumba Martin / Global Witness*

Mara kadhaa, wanakandarasi wa TotalEnergies wanasemekana kuwepo, au hata kuhusika, wakati maafisa wa Uganda walijitokeza kuwatishia watetezi kwa kuwakamata. Nelson Tibemanya, mkulima na mwanaharakati wa jamii ambaye amepigania fidia bora, alisema wawakilishi wa serikali walimtishia mara nyingi.

Alisema NewPlan alikuwepo nyumbani kwake mwaka wa 2022 wakati afisa kutoka PAU alitishia kumkamata kwa "kuhujumu" mipango ya serikali ikiwa angekataa kupokea fidia hiyo.  Usipotia saini, utaenda mahakamani...utakamatwa kwa kuzuia mradi," aliambiwa.  Nelson alikubali fidia hiyo.

"Niliathirika kisaikolojia, sikuweza kulala wakati mwingine ndani ya nyumba hiyo," Nelson alisema "Niliogopa kukamatwa - ilikuwa mateso ya kisaikolojia."

Katika kesi nyingine, mwanakandarasi wa TotalEnergies aliripotiwa kutoa tishio.  Fred Mwesigwa, mtetezi wa ardhi huko Buliisa, alisema afisa wa uhusiano wa jamii katika Atacama alimtishia kukamatwa kwa "kuhujumu programu za serikali" mnamo Julai 2020 iwapo hangekubali fidia aliyokuwa akipatiwa. Shahidi katika eneo la tukio alithibitisha kutokea kwa tukio hilo kwa Global Witness.

Takriban wanajamii kumi na wawili waliripoti kutishiwa kuchukuliwa hatua za mahakama na kampuni zinazohusika katika mradi huo.  Huko Buliisa, eneo la mradi wa kuchimba mafuta wa Tilenga unaodhibitiwa na TotalEnergies na kituo cha usindikaji, serikali imetumia maagizo ya lazima ya ununuzi kunyakua ardhi kutoka kwa jamii zinazopinga.

"Huu ni mradi wa maslahi ya umma unaofanywa na serikali ya Uganda ambayo imeamua kutumia rasilimali zake isivyofaa.  Total na EACOP hawamiliki rasilimali," mwakilishi wa timu ya EACOP alituambia katika mkutano mjini Kampala.  Watu wengine wanaweza kosa kufurahia kuhamishwa kukiwa na ununuzi wowote kama huo.  Kama Total na EACOP hazingekuwepo, [mradi] ungepewa leseni kwa mtu mwingine.  "Viwango (ambazo Kampuni iko nayo) vilivyohitajika kutwaa (ardhi) ni vya juu sana kufanywa na kampuni ya Uganda

Kupitia mawakili wake, TotalEnergies ilikanusha "kwa nguvu" kwamba TEPU na EACOP Ltd zimewatisha watu walioathiriwa kutia sahihi makubaliano yoyote ya fidia. "Badala yake, ilisoma barua kutoka Global witness, TEPU na EACOP Ltd wameweka usaidizi mwingi ili kuhakikisha kuwa PAPs wanatia Saini kwenye mikataba hii kwa hiari yao wenyewe na wanashughulikia wasiwasi huu kwa umakini wa hali ya juu.  Vitisho au unyanyasaji haviruhusiwi na zaidi ya asilimia 90% ya malalamiko yaliyowasilishwa kwa TEPU na utaratibu wa kutatua mzozo wa EACOP ulikuwa umesuluhishwa kufikia Agosti 2023.

EACOP Ltd na TEPU hawaruhusu vitisho vyovyote au unyanyasaji kwa PAPs na zinaweza kuchunguza tuhuma zozote kama hizo zilizotolewa nao. Madai yoyote ya vitisho yakiripotiwa yatachochea moja kwa moja kuanzisha uchunguzi wa ndani."Mawakili hao waliongeza kuwa madai hayo yalijaribiwa mahakamani wakati mashirika ya kiraia yalipoishtaki TotalEnergies chini ya sheria ya French Duty of Vigilance katika kesi iliyotupiliwa mbali mwaka wa 2023.  "Madai ya mashirika yasiyo ya serikali [sic] yalionekana kutokubalika na mahakama ilisema kuwa Total ilianzisha rasmi 'Mpango wa Uangalifu' kama inavyotakiwa na sheria ya Ufaransa ambayo ilijumuisha hatua za kina na za kutosha ambazo kimsingi zilitii sheria hii. "Hivyo, mahakama iligundua kuwa hakuna uvunjaji wa sheria uliokuwa umetokea."

Kwa hakika, mahakama ilitupilia mbali kesi hiyo kwa misingi ya kitaratibu na haikutoa uamuzi wa kama kulikuwa na  "msingi" wa utekelezaji wa Mpango wa Uangalifu kwa vile ulihusiisha ulinzi wa haki za binadamu na viwango vya mazingira.

> ***"Niliathirika kisaikolojia, sikuweza kulala wakati mwingine ndani ya nyumba hiyo ... Niliogopa kukamatwa - ilikuwa mateso ya kisaikolojia."***



**Mariam Najjagwe ni mfanyakazi wa kujitolea wa jamii ambaye alisema anashutumiwa kwa kueneza habari potofu na mwanakandarasi wa TotalEnergies.** *Jjumba Martin / Global Witness*

## Harakati chini ya ulinzi nchini Uganda

Nchi ya Uganda imeshikilia kampeni kali ya uhalifu, unyanyasaji na vitisho kwa watetezi wanaohamasisha kupinga mradi huo. Hii inaonekana kuwa mbinu ya kimfumo na ya makusudi ya kudhoofisha upinzani dhidi ya ukuzaji wa mafuta. Takriban watetezi 40 wanaopinga kuendelezwa kwa mradi wa mafuta au EACOP wamezuiliwa au kukamatwa nchini Uganda na serikali tangu Septemba 2020, wengine zaidi ya mara moja, kulingana na uchambuzi uliofanywa na Global Witness. Wengi wameshtakiwa kwa makosa ya kuvunja utaratibu wa umma, kama vile kero za umma, kuchochea vurugu, mkusanyiko usio halali, na mara nyingi watetezi hawa wanafungwa kwa masaa au siku kadhaa kabla ya kuachiliwa.

Lakini nambari hizi ni chache mno ikilinganishwa na mashambulizi dhidi ya watetezi wanaopinga mradi huu wa mafuta. Mashirika ya kiraia yanayosaidia wanajamii katika eneo la mafuta yalisitishwa na polisi, wakakimbia nje ya mji au wakanyanyaswa na mamlaka au 'Polisi wa Mafuta na Gesi', chombo cha usalama kisichojulikana kilichopewa jukumu la kulinda maslahi ya mafuta ya Uganda. TotalEnergies inaripotiwa kuendeleza makubaliano ya usalama na polisi wa mafuta na gesi, ingawa kwa sasa haionekani kuwepo.[7] Haipendekezwi kuwa TotalEnergies au wanakandarasi wake kwenye bomba wanawajibikia shughuli za maafisa wa serikali.

Mji wa mafuta wa Buliisa ni miongoni mwa maeneo hatari zaidi nchini Uganda ukiwa mtetezi wa mashamba na mazingira. Joss Mugisa, mwenye umri wa miaka 66, mwanzilishi wa Shirika la Haki za

Kibinadamu ya Mafuta na Gesi lililoko Buliisa, aligundua jambo hili.   Mnamo Oktoba 2021, ofisi ya shirika lake  ilivamiwa na zaidi ya watu kumi na wawili waliokuwa na silaha, wakiwemo maafisa wa serikali na polisi wa mafuta na gesi. Walichukua mafaili, vyeti vya usajili na hati kabla ya kuondoa mabango yao yaliyokuwa nje ya ofisi na kuwaambia kuwa shirika hilo limefungwa.

Muda mfupi baadaye, Mugisa alikamatwa kwa tuhuma za uwongo za uharibifu.  "Wanajua bila mimi shirika halingeendelea," Joss alisema.

Alikaa miezi sita kuanzia mwishoni mwa 2022 kwenye hali ngumu katika jela ya Buliisa, akiwa amebanwa na wanaume wengine zaidi ya kumi na wawili kwenye kibanda cha mabati, wote wakitumia ndoo moja ndogo kuoga.  Ameachwa akiwa ameumizwa na mwenye hofu akilini na pia akiugua kutokana na yaliyompata na anataka TotalEnergies ilipie huduma yake ya matibabu.  Alisema kampuni hiyo ilijua kuhusu kukamatwa kwake, lakini haikufanya lolote ” Walipokuwa wakijibu Global witness, kampuni yua TotalEnergies ilisema kuwa ilikuwa imechunguza kukamatwa kwake, lakini ikabaini kuwa "haikuhusiana na shughuli za TEPU."

> ***"Mashirika ya kiraia yanaishi kwa hofu … Wanafanya kila wawezalo kuharamisha kazi yetu."***
>
> – Mfanyakazi wa NGO

Wakati huohuo, ofisi ya Buliisa ya vikundi vingine viwili, ikiwa ni pamoja na shirika lisilo la serikali AFIEGO pia  ilifungwa.  AFIEGO ilishuhudia wafanyikazi kadhaa wakikamatwa katika kipindi cha mwaka huo, akiwemo mwanaharakati mashuhuri na mshirika wa Global Witness Maxwell Atuhura. Mmoja wa wafanyikazi wa kike wa AFIEGO huko Hoima alielezea alivyopigwa kofi na afisa ambaye aliingia ofisini kwao ghafla mnamo Aprili 2022, akamtishia na akachukua simu yake.

Mnamo mwaka wa 2021, serikali ya Ugandailisimamisha  utendakazi wa mashirika yasiyo ya serikali 54 mashirika mengi yakifanya kazi kwenye mafuta, kwa mambo kama vile kukosa kufaili kodi za mwaka au kufanya kazi bila vibali muhimu. Mtetezi wa haki za wanawake ambaye shirika lake lilikuwa kwenye orodha ya mashirika hayo, aliiambia Global Witness kwamba mamlaka sasa huchunguza shughuli zao na kutembelea ofisi yake mara kwa mara. "Sheria zimerekebishwa ili kutubana," alisema.  Katika muongo uliopita, Uganda  imeanzisha  sheria zinazozuia haki ya kuandamana pamoja na shughuli za mashirika yasiyo ya serikali.

Benon Tusingwire, mkurugenzi mtendaji katika NAVODA, alielezea alivyonyanyaswa na kupigiwa simu na vikosi vya usalama vikimhoji kuhusu hali ya usajili wa shirika lao.   Shirika lingine lisilo la serikali mjini Kampala liliambia Global Witness kuwa wametatizika kujisajili upya tangu mwanzoni mwa mwaka huu hali iliyosababisha kufanya kazi kinyume na sheria.

"Mashirika ya kiraia yanaishi kwa hofu," mmoja wa wafanyakazi wao alisema.  "Wanafanya kila wawezalo kuharamisha kazi yetu."




**Florence Nakandi amekuwa akilengwa kwa kazi yake kama mtetezi wa mazingira.** *Jjumba Martin / Global Witness*

## Matendo ya Kulipiza Kisasi dhidi ya wakosoaji wa TotalEnergies

Wanajamii wawili waliohusika katika kesi dhidi ya TotalEnergies nchini Ufaransa mnamo 2019 wanasema wamekabiliwa na vitisho na wanaishi kwa hofu na chini ya ulinzi wa kila mara. Jealousy Mugisha anatoa maelezo ya kuzuiliwa na kuhojiwa na mamlaka katika Uwanja wa Ndege wa Entebbe mnamo Desemba 2019 baada ya kurejea kutoka kwenye kesi dhidi ya Total nchini Ufaransa. Alisema walimwambia kuwa maafisa wa TotalEnergies walikuwa wamewafahamisha kuwa alikuwa mahakamani. ”Afisa wa ujasusi anadaiwa kumwambia, "Umeishtaki serikali mahakamani, unasaliti nchi yetu, wakati mwingine tutakuua. " Mapema mwaka huu, alisema gari liliigonga pikipiki yake - katika kile kilichoonekana kuwa shambulio la maksudi - na kumwacha akiwa amevunjika mguu na akihofia maisha yake.



**Jealousy Mugisha na mkewe wanaishi kwa hofu ya matendo ya kulipiza.** *Jjumba Martin / Global Witness*

Kulikuwa na majaribio mawili ya kuvunja nyumba ya Fred Mwesigwa muda mfupi baada ya kurejea kutoka Ufaransa. Hapo awali mnamo 2019, alizuiliwa na polisi na kutishiwa kufungwa jela baada ya kusaidia mtafiti wa kimataifa kuchunguza athari za bomba hilo. Mnamo 2021, alisema jeshi lilimzuia barabarani alipokuwa akirejea kutoka kwenye mkutano. "Walinitishia kwa bunduki .... wakaniambia nilale chini na wakachukua talakilishi yangu,” alisema. Tangu wakati huo, amekuwa akiishi mafichoni. "Sikai hapa nyumbani kwangu zaidi ya wiki moja ."

Mashirika mengi yasiyo ya serikali yaliyohusika katika kesi mahakamani yaliripoti kujaribu au kufaulu kuvunjwa kwa ofisi zao katika miaka ya hivi karibuni, katika baadhi ya kesi hati za ushahidi zilizohitajika kupelekwa mahakamani zilitoweka.

Kulingana na Florence Nakandi, shirika lake lisilo la serikali la COTFONE mara nyingi huwaona watu wasiojulikana wakichunguza ofisi zao. Wanaharakati wengi tuliowahoji waliogopa kuwa walikuwa wakifuatiliwa kupitia uchunguzi wa simu au programu ya upelelezi.

Inaripotiwa kuwa kundi lingine lililohusika katika kesi dhidi ya EACOP katika Mahakama ya Afrika Mashariki lilipigiwa simu kutoka kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiwaonya kuondoa kesi hiyo. Miezi michache iliyopita, maafisa waliwahoji kuhusu hali yao ya usajili. “Je, kwa nini mnafuatilia kesi ya EACOP? Unatakiwa kuwa mwangalifu sana, usiwe mtu wa kuihujumu serikali,” David Kabanda, kutoka kituo cha Chakula na Haki za Maisha, alikumbuka akiambiwa hivo kwa wakati huo.

Kuna sababu za kuchunguza iwapo TotalEnergies na mamlaka ya Uganda wanasambaziana taarifa kuhusu wanaharakati. Kama ilivyo katika kesi ya Jealousy Mugisha, kuna ripoti ambazo hazijathibitishwa ambazo zinaweza kupendekeza uhusiano unaofaa kati ya kuchukua hatua ya upinzani dhidi ya TotalEnergies na matendo ya kulipiza kisasi yaliyofanywa baadaye na asasi za serikali.

Kiongozi wa jamii katika sehemu moja ya mradi wa bomba la mafuta, ambaye alikamatwa kwa mara ya kwanza Oktoba 2021 na kushtakiwa kwa kuhujumu miradi ya serikali, sasa anaishi mafichoni. Ana malalamiko ambayo hayajatatuliwa na TotalEnergies. Mnamo Julai 2023, baada ya siku tatu za

mazungumzo ambayo hayakufanikiwa na wawakilishi wa kampuni, alisema aliitwa kwenye mkutano na afisa wa serikali ya mitaa. Hakuenda kwa sababu alihofia kukamatwa tena. Muda mfupi baadaye, wanaume wawili walifika nyumbani kwake usiku wa manane wakimtafuta, mke wake alimwambia. Kwa bahati nzuri, hakuwepo kwani ni mara chache yeye hulala kwake. "Naogopa kwenda kulala nyumbani na huwa nalala msituni."

Mwanaharakati mmoja kutoka Buliisa alikumbuka wakati alipogundua kwamba jina lake lilikuwa kwenye "orodha ya watakaokamatwa" kutoka kwa mtu aliyemfahamu ambaye alihudhuria mkutano na maafisa wa serikali na kampuni ya TotalEnergies. “Alinipigia simu kuniambia ni lazima nijifiche kwani wanakuja kunikamata.”

Maxwell Atuhura anaamini kuwa kampuni ya mafuta ya TotalEnergies lazima iwajibike kwa jukumu analodai ilitekeleza katika kukamatwa kwake mnamo Mei 2021. Akiwa kizuizini, alimkumbuka Kamanda wa Polisi wa Mafuta na Gesi, ambaye kampuni ya TotalEnergies inashirikiana naye kwa ukaribu, akija kumhoji. “Je, una uhusiano gani na kampuni ya Total? Mbona wananiuliza mengi kukuhusu?” alisema kuwa aliulizwa hivo. "Usipoacha utateseka.” Yeye ni miongoni mwa walalamishi kadhaa wanaoishtaki kampuni ya TotalEnergies nchini Ufaransa chini ya sheria ya Duty of Vigilance ya nchi hiyo kwa vitisho na unyanyasaji anaokabiliana nao akipinga EACOP.

Katika barua kwa Global Witness, TotalEnergies ilisisitiza kuwa iliwasilisha kesi ya Maxwell kwa mamlaka ya Uganda. Pia walibaini uhusiano wake wa awali na AFIEGO, shirika ambalo walilieleza kuwa "halijasajiliwa" na lilijihusisha na shughuli ambazo "hazijaruhusiwa". "Hili ni suala linalohitaji mazungumzo na mamlaka ya Uganda."

Kuhusu kesi ya Mugisha kampuni ya TotalEnergies ilisema kuwa haikuwa na ufahamu juu ya kuzuiliwa kwake na kwamba alijitokeza hadharani katika mkutano na waandishi wa habari kuhusu kesi hiyo ya mahakama ya Ufaransa.

## Kesi kadhaa za watu kukamatwa

Wanaharakati kadhaa wa hali ya hewa wamekamatwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kwa ajili ya kufanya maandamano dhidi ya EACOP.

Baadhi yao wamepigwa wakiwa vizuizini. Wengi wameshtakiwa kwa kukusanyika kinyume cha sheria chini ya sheria kali ya kupambana na maandamano iliyotumiwa dhidi ya wapinzani wa serikali. Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa na Bunge la Umoja wa Ulaya wamelaani unyanyasaji wa watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi kwenye mafuta na gesi.

Lakini katika mkutano na Global Witness, timu ya EACOP ilipuuza madai ya mashambulizi dhidi ya mashirika ya kiraia. "Kila mara tunaposikia madai ya ukiukaji wa haki za binadamu, huwa tunachunguza.... Lakini hakuna ushahidi kwamba madai haya ni sahihi.”

"Serikali inaweza kuwakamata [wanaharakati] kwa 'shughuli zisizo halali' kama wanavyoweza katika nchi yoyote… Hatuhukumu. Sio jukumu letu kuamua iwapo watu wamekamatwa kwa haki au la. Mwakilishi aliongeza kuwa mara nyingi hakukuwa na ushahidi kwamba wizi wa aina hiyo ulifanywa na serikali.

"Uganda ni nchi huru. Je, umepata matatizo yoyote ukija hapa kuripoti? Hujasumbuliwa. Nchi zote zinazopakana na Uganda hazina uhuru zaidi.”




**Wanafunzi wanne walikamatwa kwa nguvu mnamo Septemba 2023 kwa kuandamana dhidi ya EACOP.** *REUTERS*

## Tanzanie : suppression de l'espace civique

Awali, EACOP ilikusudiwa kufika pwani ya Kenya, lakini inaripotiwa kuwa kampuni ya Total energies ilishinikiza ipitie Tanzania. Uamuzi huo umeibua maswali kutokana na mazingira ya kutumia nguvu za kimabavu zaidi ya kisiasa nchini Tanzania. Chini ya uongozi wa hayati rais John Pombe Magufuli, haki za raia wa Tanzania zilipungua, kutokana na kupigwa marufuku kwa mikutano ya kisiasa, na vikwazo vikali kwa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza. Urithi wake na Rais Samia Suluhu Hassan mnamo 2021 umeleta maboresho, lakini hali ya ukandamizaji bado ipo.

Nchini Tanzania rais anamiliki ardhi yote jambo ambalo limefanya iwe rahisi kwa Kampuni ya EACOP kumiliki ardhi (na inadai kuwa imeweza kukamilisha asilimia 99 ya mikataba ya fidia). Lakini uchunguzi wetu unapendekeza kwamba kampuni hii ya mafuta imefaidika, kwa makusudi au vinginevyo, kutoka kwa nafasi ya siasa za kimabavu na ukandamizwaji wa uhamasishaji wa mashirika ya kiraia yaliyo karibu na bomba hilo la mafuta. Kuna marufuku madhubuti ya uanaharakati unaochukuliwa kuwa 'upinzani wa serikali' ambayo imetumika kuwanyamazisha watetezi wa ardhi na wapinzani wa EACOP.

Wanajamii wengi tuliowahoji hawakuweza kupata usaidizi kutoka kwa mashirika ya kiraia na wale waliofanya hivyo mara nyingi waliogopa kukutana nao. Baadhi yao walipelekwa mbele ya mamlaka na kuhojiwa kuhusu uhusiano wao na makundi ya asasi za kiraia na iwapo walipinga EACOP. Mwanamume mmoja kutoka Tanga alisema kuwa wanajamii wanahitaji ruhusa kutoka

kwa timu ya EACOP ili kukutana na mashirika ya asasi za kiraia, Kimsingi, mashirika ya kiraia yanayounga mkono serikali yanapendelewa.[8]

“Hatuna huru, huwa tunajificha tunapokutana na watu kutoka CSOs. Hatuna uhuru wa kujadili waziwazi masuala yoyote kwa sababu mara zote tukifanya hivyo huwa tunajikuta mikononi mwa maafisa wa polisi", alisema Aziza Bilaa, mkulima kutoka Dodoma. Alitembelewa na maafisa wawili wa polisi aliporejea kijijini mwake kutoka kwa hafla ya mabadiliko ya hali ya hewa nchini Kenya. Alipelekwa haraka kwenye kituo kilicho karibu cha na kuhojiwa na polisi na maafisa wa serikali ya mtaa.

“Je, ulikuwa unatoka wapi? Je, ulifanya nini?”, alikumbuka akiulizwa alipokuwa kizuizini kwa muda wa masaa matatu. "Nitakuonya usifanye chochote ambacho ni kinyume na mradi huo.”

Tukio hilo lilimfanya aogope sana kiasi cha kutaka kuhama.

Ni makundi machache tu yanaonekana kufanya kazi bila ya serikali na jamii zilizoathiriwa na mradi huo, na yanakabiliwa na vikwazo vingi. Ni lazima yafanye kazi kwa kujificha katika jamii au yaingie katika hatari ya kutishwa, kukamatwa au kufukuzwa na maafisa wa serikali.

"Kila unapogusa mafuta, unagusa makampuni tajiri na maslahi ya serikali.

Ukigusa suala la serikali unaweza kutoweka,” alisema mwanaharakati ambaye aliomba kutotajwa.

Makundi na wanaharakati wachache waliojitokeza wametishwa, kukamatwa na kunyanyaswa na mamlaka.

Richard Senkondo na Baraka Lenga, ambao ni watetezi wa mazingira, walilazimika kuikimbia nchi mapema mwaka huu baada ya kuandaa mkutano na waandishi wa habari jijini Arusha ambao uliibua wasiwasi kuhusu EACOP. Hakuna hata mmoja wa waandishi wa habari waliokuwepo aliyeripotiwa kuandika kisa hicho. Lakini jioni hiyo hiyo watetezi walitumiwa ujumbe na kupigiwa simu wakiambiwa "wajihadhari" kwa "kwenda kinyume na serikali". Ujumbe huo ulitaja hata jina la hoteli waliyokuwa wakiishi. Kwa hofu, walizima simu zao, wakafunga virago vyao na kuvuka mpaka wa nchi kuelekea Kenya. Waliporudi nyumbani wiki chache baadaye, polisi waliwakuta katika nyumba zao.

Nyumba zao zilipekuliwa, kompyuta na simu zao zilichukuliwa.

***"Ukigusa suala la serikali unaweza kutoweka.”***

– Mwanaharakati ambaye aliomba kutotajwa.

Richard amelazimika kuhamishia ofisi ya shirika lake la Organization for Community Engagement hadi nje ya jiji la Dar es Salaam kufuatia ziara za mara kwa mara za polisi kuwashambulia na kuwatisha wafanyakazi wake wa kujitolea. Richard alieleza: "Polisi wangewaambia wafanyakazi hao wa kujitolea: “Nyinyi bado ni wadogo sana, mnaweza kupoteza maisha yenu mkiwa gerezani,”

"Huu ni mradi mzuri, tutapata pesa .... Je, kwa nini mnaupinga mradi huu?" Watu hao wote watatu wa kujitolea walijiuzulu ndani ya siku chache.

Wale wanaoonekana kuwasaidia waandishi wa habari au watafiti wa kimataifa hasa wanaonekana kuwa hatarini. Baraka Lenga alilazimika kuripoti kwa polisi mnamo Machi 2022 baada ya kumsaidia mtafiti wa kimataifa kuchunguza bomba hilo la mafuta. "Unahitaji kuacha kuipinga serikali," polisi walimwambia akiwa kituoni. "Ikiwa unataka kazi, tunaweza kukupa moja, kazi nzuri."

Baraka Machumu, mtetezi mwingine ambaye shirika lake la Green Conservers lilishirikiana na Global Witness kwenye utafiti huu, amenyanyaswa. Mnamo Julai 2022, alikuwa amepanga ziara ya nyanjani kwa waandishi wa habari wawili wa Italia wanaoandika juu ya EACOP, kabla ya kujaribu kupata mikutano na kampuni hiyo ili kuwauliza maswali. Baada ya kunyimwa nafasi katika ofisi ya EACOP, walisimama mlangoni katika ofisi ya TotalEnergies, Dar es Salaam, ambapo ofisa mmoja wa usalama alimzuilia Baraka ofisini mwake na kumhoji huku akiitisha simu na kitambulisho chake. “Tayari tunajua kuwa ulifika katika ofisi yetu ya EACOP. Tunajua kuwa unaandika kitu kibaya kuhusu mradi huo,” anakumbuka afisa wa usalama akimwambia. "Nitazidi kukuchunguza," aliambiwa kabla ya kuachiliwa.[9]

Siku mbili baadaye, aliona mtu akimfuata. Kiongozi wa eneo hilo alimwambia kwamba watu fulani walikuwa wakiuliza habari kumhusu na kuhusu watu aliofanya kazi nao. Baadaye usiku huo, alisikia mlango wake ukibishwa. Kwa hofu, hakujibu na muda mfupi baadaye alitoweka kutoka nyumbani kwake, na baadaye akaikimbia nchi.

Mwaka uliotangulia, alifunga afisi yake baada ya uvamizi uliomuacha akihofia kuingiliwa na serikali.

Mwalimu mmoja wa zamani aliliambia shirika la Global Witness kwamba alipoteza kazi yake katika shule ya serikali kwa kukosoa waziwazi EACOP. Kwa sasa yeye ni mwanaharakati huru, anapendelea kujiita "mwanasheria" ili kuepuka kuitwa mpinga serikali.

Kampuni TotalEnergies ilisema "haiwezi kuwajibishwa" kwa matendo ya wahusika wengine na ilikanusha vikali uhusiano wowote na "tabia iliyo kinyume cha sheria".

## Kudhoofisha Uwajibikaji

Swalehe ni mmoja wa waombaji 50 wanaotarajiwa nchini Tanzania katika malalamiko ya kisheria dhidi ya makampuni yanayohusika katika ujenzi wa bomba hilo la mafuta, ikiwemo Kampuni ya EACOP iliyosajiliwa Uingereza. Kulingana na malalamiko hayo, wanajamii wengi walipokea notisi za kufukuzwa mnamo 2023, baada ya kulipwa fedha kidogo kwa ajili ya ardhi yao.

Muda mfupi baada ya kuwasilisha notisi hiyo ya kisheria, wanajamii waliripoti mamlaka ya eneo hilo iliwasiliana nao wakiwauliza wanafanya kazi na nani. Swalehe alipigiwa simu na kumuita kwenye ofisi ya ofisa wa serikali ya mtaa. Je, kwa nini mnaupinga mradi huu?" Je, nani anayewafadhili?” ofisa huyo aliuliza. Wawakilishi wa mashirika ya kiraia waliohusika katika kesi hiyo wanasema waliwasiliana na wanajamii wengine ambao walikuwa wamenyanyaswa na viongozi wa eneo hilo.

Makundi yanayojenga kesi tofauti dhidi ya EACOP katika Mahakama ya Afrika Mashariki yamepata ugumu kupata ushuhuda kutoka Tanzania. Kulingana na mawakili waliohusika katika kesi hiyo, mashahidi wamekuwa wakisita kutoa ushahidi wao, wakitaja wasiwasi kuhusu kulipiziwa kisasi.

"Watu wengi walipata tu fidia zao mapema mwaka huu - na sasa wameanza kutambua kuwa walikuwa wanalipwa kiasi kidogo," alielezea Richard Senkondo, ambaye alipigiwa simu kutoka kwa watu ambao wana wasiwasi "kwa sababu sasa wanajaribu kununua ardhi ila hawawezi.

## Athari ya Kutamausha

Matendo ya kulipiza kisasi yamekuwa na athari mbaya ya kutamausha kwa jamii zilizo katika mstari wa mbele na jamii ya kiraia nchini Uganda na Tanzania. Utafiti wetu unaonyesha kwamba jamii zimesitisha juhudi za kupinga kampuni hiyo juu ya ununuzi wa ardhi, wakati wanaharakati wengine wamepunguza utetezi au wameepuka kulipinga bomba hilo la mafuta kabisa.

Mkaundi mawili ya asasi za kiraia kutoka Uganda yalikataa kushiriki katika kesi ya pili dhidi ya TotalEnergies nchini Ufaransa, yakitaja masuala ya usalama.

Mtetezi mmoja wa kike alisema amepunguza juhudi zake za utetezi dhidi ya EACOP kutokana na shinikizo, badala ya fidia bora na haki kwa wanawake. "Huwezi kutetea chochote ukiwa umekufa," alisema. Mwanaharakati mwingine wa kike alielezea kuwa alipata "mateso ya kisaikolojia", huku familia yake ikiishi kwa hofu. Wengine wamejificha au kuhama kila mara kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine ili kuepuka kunyanyaswa na wenye mamlaka.



**Une femme montre un avis d’expulsion envoyé par Tanzania Petroleum Development Corporation**. (Green Conservers)

***"Ni gharama kubwa sana kusema 'Sitisha EACOP'. »***

– Mkurugenzi Mtendaji wa NGO

Vikundi vya wanaharakati vimepoteza wafanyakazi - wakati mwingine kwa kampuni hiyo ya mafuta yenyewe - na ari imepungua. Hatari za kuandaa maandamano ya amani dhidi ya EACOP zimewafanya wanaharakati wengi nchini Uganda na Tanzania kuingia mtandaoni, jambo ambalo linafungua njia mpya za uhamasishaji na utetezi, pamoja na vitisho na ufuatiliaji.

Mtanzania mmoja ambaye ni mfanyakazi huru alisema amefungiwa kufanya kazi na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania kwa sababu ya utetezi wake dhidi ya EACOP. Mahojiano na vikundi vikubwa vya mabadiliko ya hali ya hewa nchini Tanzania yalionyesha kutotaka kabisa kufanya kazi kwenye mafuta ya kisukuku - achilia mbali EACOP - ili kuepuka kuikasirisha serikali. Kikundi kimoja kikuu cha hali ya hewa kinasema kiliagizwa na maafisa wa serikali kutofanyia kazi mafuta ya kisukuku. Badala yake, vikundi vingi vya hali ya hewa huzingatia tu kukuza nishati mbadala, lakini huepuka kutaja nishati ya kisukuku.

"Ni vigumu kutoa wito wa kusimamisha mradi huo wa mafuta," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika Lisilo la serikali la Uganda, ambaye aliomba kutotajwa jina kwa misingi ya usalama. “Utanyanyaswa, utatishwa, wafanyakazi watapoteza kazi zao. "Ni gharama kubwa sana kusema 'Sitisha EACOP'.

## Hitimisho

Uwezekano wa kampuni ya TotalEnergies kushiriki katika ulipizaji kisasi dhidi ya wale waliopinga EACOP nchini Uganda na Tanzania uliofanywa na mawakala wa serikali unastahili uchunguzi zaidi. Uchunguzi wetu ulifichua ushahidi ambao unaonyesha kuwa wawakilishi wa kampuni wanaweza kuwa wameshiriki habari kuhusu watetezi maalum na mamlaka za serikali. Iwapo hili limefanywa kwa ufahamu au nia ambayo itafanya ulipizaji kisasi kufuata (ambao kwa sasa hakuna ushahidi), hili linaweza kuifanya kampuni kuwajibika. Angalau, kampuni hiyo kubwa ya mafuta inaonekana imeshindwa katika uchunguzi wake wa athari za haki za binadamu kwa kufanya biashara na mataifa mawili ya kidikteta. Kampuni hiyo imejaribu kupunguza uzito wa mashambulizi kwenye maeneo ya kiraia, ambayo yanaweza kuwaweka kinyume na majukumu yao chini ya Kanuni Elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Kibinadamu. Zaidi ya hayo, ushiriki wowote wa moja kwa moja katika uonevu na vitisho kwa jamii ili kukubali mikataba ya fidia kunaweza kujumuisha ukiukaji wa mikataba hii. Vile vile kutakiuka viwango vya kimataifa.

Mashirika ya kiraia nchini Tanzania na Uganda yamegawanyika kuhusu jinsi ya kuendelea na suala la EACOP. Baadhi ya makundi yanasema kuwa yamechelewa sana kusimamisha mradi huo na wanataka kuangazia uboreshaji wa manufaa kwa jamii za eneo hilo. Makundi mengine yanasema kuwa mradi huo hauwezi kuendelezwa kwa njia endelevu. Vyovyote vile, mazungumzo yameharibiwa na ukandamizaji wa kisiasa, hili linaleta hatari ya kudhoofisha mpito wa kimataifa kuelekea kiasi cha sifuri cha uharibifu wa hali ya hewa.

“Kunapaswa kuwa na mjadala juu ya EACOP,” alisema Onesmus Mugyenyi, kutoka Muungano wa Mawakili wa Maendeleo na Mazingira. "Sio kuwanyamazisha watu.”

## Mapendekezo

Matokeo yetu yanaonyesha hitaji la hatua ya kimataifa ya kuwalinda watetezi na haki za binadamu katika muktadha wa mabadiliko ya hali ya hewa. Mapendekezo yaliyo hapa chini yameandaliwa pamoja na watetezi wa mazingira katika Afrika Mashariki.

### Wanachama katika Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa (UNFCCC):

> Kutambua jukumu la watetezi katika kuendeleza hatua za kutunza hali ya hewa na kuchukua hatua za maana ili kulinda watetezi na nafasi ya kiraia (mtandaoni na ana kwa ana) ili kukuza hatua za kutunza hali ya hewa.

> Kuhakikisha ushiriki wa maana na wenye ufanisi wa watetezi wa ardhi, mazingira na haki za binadamu, pamoja na watu wa asili na jamii zilizo katika hatari katika kupanga, kubuni na utekelezaji wa maamuzi na michakato **yote** muhimu inayohusiana na utekelezaji wa Mkataba wa Paris na katika uundaji wa sera za kulinda hali ya hewa ikiwa ni pamoja na kupata mabadiliko ya haki ya nishati na kukuza hatua za utunzaji wa hali ya hewa zinazozingatia haki za binadamu.

### Nchi za Uganda na Tanzania

> Kulinda haki za ardhi na haki za binadamu za jamii zinazoathiriwa na maendeleo katika sekta ya mafuta, ikiwa ni pamoja na kutekeleza kanuni ya ridhaa ya bure, ya awali na ya taarifa (FPIC), na kuhakikisha kwamba watu walioathirika wanalipwa fidia ya haki kwa ardhi na mali zao, na kwamba wanafikia mifumo huru ya malalamiko na masuluhisho ya madhara

> Ruhusu ufikiaji wa bure na kamili kwa maeneo ya mafuta na bomba kwa mashirika ya kiraia, waandishi wa habari wa kujitegemea na watafiti.

> Kwa kushirikiana na mashirika ya kiraia na wataalam, kuanzisha na kutekeleza taratibu za kisheria za ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu kulingana na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu.

> Kuondoa vizuizi vya uharakati wa hali ya hewa na haki ya kupinga EACOP na miradi mingine ya mafuta ya kisukuku.

> Kujitolea hadharani kulinda watetezi wa ardhi, mazingira na haki za binadamu kama sehemu ya mipango ya kitaifa ya mabadiliko ya nishati, na kuchukua hatua za maana za kuhusisha mashirika ya asasi za kiraia na jamii za mitaa katika mazungumzo ili kukabiliana na mgogoro wa hali ya hewa na kukuza ufumbuzi wa nishati mbadala.

**Uganda:**

> Kutanguliza vipengee vya ulinzi kwa sheria iliyopo ambayo inaweza kutumika vibaya kuwatia hatiani watetezi, huku sheria zinazowalenga waandamanaji na kuwafanya waonekane kuwa wahalifu zinapaswa kubatilishwa. Hatua ya kubatilisha au kurekebisha sheria zinazotumika kukandamiza uhuru wa kujieleza na nafasi ya kiraia, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

(2016), Sheria ya Kudhibiti Amani ya Umma (2013), Sheria ya Matumizi Mabaya ya Kompyuta (2011) na vifungu vya kukashifu kwa jinai.

> Kuimarisha mahakama ili iweze kusikiliza na kuhitimisha kesi za haki za binadamu na mazingira kwa wakati.

> Komesha polisi kutumia nguvu kunyanyasa na kutisha watetezi wa mazingira na haki za binadamu

**Tanzania:**

> Kutanguliza vipengee vya ulinzi kwa sheria iliyopo ambayo inaweza kutumika vibaya kuwatia hatiani watetezi, huku sheria zinazowalenga waandamanaji na kuwafanya waonekane kuwa wahalifu zinapaswa kubatilishwa.

> Kuondoa au kurekebisha sheria zinazotumiwa kupunguza uhuru wa kusema na nafasi ya kiraia ili kuhakikisha ulinzi mkubwa kwa watetezi wa ardhi, mazingira na haki za binadamu. Hii ni pamoja na: Sheria ya Makosa ya Mtandao ya (2015), Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya (2016), Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni) (2020), Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu (1994), Sheria ya Utumizi wa Pesa Haramu ya (2006) na Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya (2002)

### Kampuni ya TotalEnergies

> Inapaswa kupitisha, kuchapisha na kutekeleza msimamo wa sera kuhusu watetezi wa ardhi na mazingira, na kuhakikisha kuwa hii inaingizwa katika mifumo na sera za usimamizi wa kampuni hiyo kulingana na Kanuni za Umoja wa Mataifa za Biashara na Haki za Kibinadamu ikiwa ni pamoja na tathmini ya hatari ya kulipiza kisasi na uchunguzi kabla na katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi huo.

> Kutekeleza sera ya FPIC kama ilivyoainishwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Wenyeji wa Asili, Mkataba wa ILO 169 na Miongozo ya Hiari ya Umoja wa Mataifa juu ya Utawala Wajibikaji wa Umiliki wa Ardhi, Uvuvi na Misitu. Hii inapaswa kujumuisha kuheshimu haki za jamii zilizoathiriwa na mafuta za kusema hapana kwa EACOP na Tilenga

> Itumie mbinu ya "kutovumilia kabisa" matendo ya kulipiza kisasi na vitisho, na itumie nguvu zake kushinikiza mamlaka ya Uganda na Tanzania kulinda na kuheshimu watetezi wa mazingira na hali ya hewa

> Kutathmini hatari kwa sera na desturi za wanakandarasi na wanakandarasi wadogo kuhusiana na masuala ya LED mara kwa mara. Kuwasaidia wanakandarasi kuimarisha nafasi zao za sera na hatua zinazohusiana na LED, inapohitajika.

> Kuchunguza madai ya wafanyakazi na wanakandarasi kushiriki kwa kuhusiana na watetezi wa ardhi na mazingira mara kwa mara. Saidia wanakandarasi kuimarisha misimamo yao ya kisera na vitendo vinavyohusiana na watetezi wa ardhi na mazingira inapobidi.

> Kutekeleza taratibu au itifaki za kiwango cha utendakazi za malalamiko ambazo zinashughulikia na ziko tayari kukabiliana na, hali mahususi ya malalamiko ya watetezi wa haki za binadamu, ardhi na

mazingira.

> Kuendelea kushirikisha na kufuatilia washikadau walioathiriwa na miradi ya uchimbaji mafuta ya EACOP ama miradi ingine inayohusiana na kuchimba mafuta.

> Kushirikiana kikamilifu na vyombo vya kisheria vya kimataifa vinavyochunguza ushiriki wake katika ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusishwa na EACOP na Tilenga

> Kutanguliza mpito wa kweli, wa haki na wa haraka kutoka kwa utumizi wa mafuta ya kisukuku hadi kwa teknolojia ya nishati mbadala.

**Taasisi za Fedha Duniani**

> Zikatae kufadhili miradi iliyozama katika ukiukaji wa haki za binadamu au kukosa idhini ya bure, ya awali na ya baada ya kupashwa habari kutoka kwa jamii zilizoathiriwa, au ambayo inashindwa kukidhi viwango vya kimataifa vya haki za binadamu kwenye sekta ya fedha.

> Ziongeze uwekezaji katika sekta za nishati mbadala na teknolojia

> Ziunge mkono juhudi za kuanzisha mahitaji ya lazima ya udhibiti wa haki za binadamu na mazingira kwa makampuni, ikiwa ni pamoja na chini ya pendekezo la Umoja wa Ulaya la Mwongozo wa Uchunguzi wa Uendelevu wa Kampuni

**Umoja wa Ulaya**

> Kutekeleza agizo dhabiti na kabambe juu ya uchunguzi wa lazima wa shirika kulingana na viwango vya kimataifa na ambalo linahitaji kampuni kutathmini na kushughulikia athari zao mbaya kwa haki za binadamu, mazingira na hali ya hewa. Sheria inayopendekezwa ya uchunguzi (Mwongozo wa Uchunguzi wa Uendelevu wa Kampuni) inapaswa:

>> Kuelekeza makampuni kufanya ushirikiano salama, wa maana na unaoendelea na washikadau ambao wanaweza kuathiriwa na shughuli za kampuni. Ushiriki huu lazima uzingatie athari tofauti kwa vikundi vilivyo hatarini ikiwa ni pamoja na wanawake na watu wa kiasili

>> Kuhakikisha kuwa watu na jamii zilizoathiriwa zinaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya kampuni kwa madhara yanayotokana na shughuli za kibiashara. Hatua hizi lazima zishughulikie vizuizi vya kupata haki katika Mahakama za Ulaya na kuhakikisha kwamba wale walioathiriwa wanapatiwa fidia inayofaa, kulingana na viwango vya kimataifa.

>> Kuelekeza makampuni kuunda na kutekeleza mipango ya mpito ambayo inalingana na malengo na matarajio ya Mkataba wa Paris na kujumuisha upeo wao wa 1, 2 na 3 wa uzalishaji.

# Références


[1] Mahojiano ya Global Witness na Green Conservers na watu walioathirika kutokana na mradi Tanzania; 2023.

"EACOP: A Disaster in the Making", Les Amis de la Terre France, October 2022 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2022/10/eacop-a-disaster-in-the-making-foe-france-and-survie-oct-2022.pdf

Global Witness, Green Conservers and Tasha Research Institute interviews with project-affected persons in Uganda and Tanzania; 2023.

EMPTY PROMISES DOWN THE LINE? A Human Rights Impact Assessment of the East African Crude Oil Pipeline, Oxfam, p.58 https://oxfamilibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621045/rr-empty-promises-down-line-101020-en.pdf?sequence=1&isAllowed=y

New Oil, Same Business? At a Crossroads to Avert Catastrophe in Uganda, International Federation for Human Rights, 2020, p.64 https://www.fidh.org/IMG/pdf/fidh__fhri_report_uganda_oil_extraction-compresse.pdf

EACOP: A Disaster in the Making, Amis de la Terre, 2022, p.12 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2022/10/eacop-a-disaster-in-the-making-foe-france-and-survie-oct-2022.pdf

[1] Global Witness, Green Conservers and Tasha Research Institute interviews with project-affected persons in Uganda and Tanzania; 2023.

[1] Global Witness, Green Conservers and Tasha Research Institute interviews with project-affected persons in Uganda and Tanzania; 2023.

EACOP: A Disaster in the Making, Amis de la Terre, 2022, pp.15-17 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2022/10/eacop-a-disaster-in-the-making-foe-france-and-survie-oct-2022.pdf

Our Trust is Broken, Human Rights Watch, 2023 https://www.hrw.org/report/2023/07/10/our-trust-broken/loss-land-and-livelihoods-oil-development-uganda#_ftn45

EMPTY PROMISES DOWN THE LINE? A Human Rights Impact Assessment of the East African Crude Oil Pipeline, Oxfam, p.58 https://oxfamilibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621045/rr-empty-promises-down-line-101020-en.pdf?sequence=1&isAllowed=y

New Oil, Same Business? At a Crossroads to Avert Catastrophe in Uganda, International Federation for Human Rights, 2020, p.64 https://www.fidh.org/IMG/pdf/fidh__fhri_report_uganda_oil_extraction-compresse.pdf

"A Nightmare Named Total », Les Amis De La Terre, 2020 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2020/11/a-nightmare-named-total-oct2020-foe-france-survie.pdf

[1] "Literacy rate, adult total (% of people ages 15 and above)", World Bank, 2022 https://data.worldbank.org/indicator/SE.ADT.LITR.ZS

[8] Mahojiano ya Global Witness na Green Conservers na watu walioathirika kutokana na mradi Tanzania; 2023.

"EACOP: A Disaster in the Making", Les Amis de la Terre France, October 2022 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2022/10/eacop-a-disaster-in-the-making-foe-france-and-survie-oct-2022.pdf

Global Witness, Green Conservers and Tasha Research Institute interviews with project-affected persons in Uganda and Tanzania; 2023.

EMPTY PROMISES DOWN THE LINE? A Human Rights Impact Assessment of the East African Crude Oil Pipeline, Oxfam, p.58 https://oxfamilibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621045/rr-empty-promises-down-line-101020-en.pdf?sequence=1&isAllowed=y

New Oil, Same Business? At a Crossroads to Avert Catastrophe in Uganda, International Federation for Human Rights, 2020, p.64 https://www.fidh.org/IMG/pdf/fidh__fhri_report_uganda_oil_extraction-compresse.pdf

EACOP: A Disaster in the Making, Amis de la Terre, 2022, p.12 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2022/10/eacop-a-disaster-in-the-making-foe-france-and-survie-oct-2022.pdf

[9] Global Witness, Green Conservers and Tasha Research Institute interviews with project-affected persons in Uganda and Tanzania; 2023.

[9] Global Witness, Green Conservers and Tasha Research Institute interviews with project-affected persons in Uganda and Tanzania; 2023.

EACOP: A Disaster in the Making, Amis de la Terre, 2022, pp.15-17 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2022/10/eacop-a-disaster-in-the-making-foe-france-and-survie-oct-2022.pdf

Our Trust is Broken, Human Rights Watch, 2023 https://www.hrw.org/report/2023/07/10/our-trust-broken/loss-land-and-livelihoods-oil-development-uganda#_ftn45

EMPTY PROMISES DOWN THE LINE? A Human Rights Impact Assessment of the East African Crude Oil Pipeline, Oxfam, p.58 https://oxfamilibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621045/rr-empty-promises-down-line-101020-en.pdf?sequence=1&isAllowed=y

New Oil, Same Business? At a Crossroads to Avert Catastrophe in Uganda, International Federation for Human Rights, 2020, p.64 https://www.fidh.org/IMG/pdf/fidh__fhri_report_uganda_oil_extraction-compresse.pdf

"A Nightmare Named Total », Les Amis De La Terre, 2020 https://www.amisdelaterre.org/wp-content/uploads/2020/11/a-nightmare-named-total-oct2020-foe-france-survie.pdf

[9] "Literacy rate, adult total (% of people ages 15 and above)", World Bank, 2022 https://data.worldbank.org/indicator/SE.ADT.LITR.ZS